

# MUHTASARI WA KISERA

## Wajibu wa Kimataifa, uwajibikaji ndani ya nchi



**Usimamizi wa maliasili** katika muongo mmoja uliopita umeunda kiunzi shirikishi, ambacho kimewashirikisha wanawake na jamii, na kimetoa manufaa kwa watuamiaji wenyeji. Hata hivyo, ukataji haramu wa magogo umekuwa ukiendelea; ukosefu wa usawa wa kijinsia umekithiri; ukosefu wa uwazi na usawa katika ugawaji wa manufaa; migogoro imeongezeka katika maeneo mengi; na mifumo ya utekelezaji ni dhaifu. Utafiti wetu kuhusu juhudhi za usimamizi wa maliasili katika nchi za Nepal, Meksiko, na Tanzania tangu mwaka 2012 umeweza msisitizo kwa watendaji, washiriki, na mikakati ya usimamizi. Kwa kuzingatia kazi yetu, tumepata matokeo bora zaidi kwa kuweka msisitizo katika (1) matokeo na mienendo ya kimuktadha mahususi, (2) ugawaji wa faida, gharama, na vihatarishi, na (3) dhima za watendaji wa kisera, sekta binafsi, vikundi vyta watumiaji wa misitu na wananchi, hususani makundi maalum kama vile wanawake na vijana.

**Tunaona pia kuwa** juhudhi za usimamizi wa maliasili zinaendelea kutegemea mantiki mpya ya kuwafanya watumiaji wenyeji na wafanyamaamuzi wajibike kwa ustawi wao na uendelevu wa maliasili. Juhudi hizi zinatarajia kwamba wananchi, jamii, na wafanyamaamuzi wenyeji watatekeleza majukumu na wajibu mpya bila kuangalia kikamilifu uwezo wao. Katika muktadha huu unaobadilika, utafiti wetu unasisitiza umuhimu wa kutafuta njia za kupima uwajibikaji wa kimataifa na ule wa ndani ya nchi.

**Ushiriki wa umma** katika usimamizi wa maliasili unaweza kutazamwa, kwanza kama zana ya kupatia matokeo bora; na pili, kama mchakato wa lengo. Usimamizi wa rasilimali kama mchakato unapaswa kuwa jumuishi kwa kuzingatia maslahi na kujitolea, ambapo matakwa ya kisheria yanaweza kujalizia. Hata hivyo, baadhi ya watu wanaweza kushindwa kushiriki kutokana na kukosa taarifa, maslahi, imani, au ruksa, au kwa sababu tu wana mbinu zingine zinazoweza kuathiri maamuzi. Tofauti ya haki ya kuchagua kutokushiriki na kushindwa kushiriki kutokana na kukosa uwezo inahitaji kuangaliwa kwa umakini mkubwa vilevile.

Usimamizi wa maliasili unaimarishwa kwa kuwezesha fursa mbalimbali za wananchi wote walio tayari kushiriki na wananchi wanaoweza kushiriki kwa kuzingatia uwezo wao. Uwezo wa namna mbalimbali unaweza kujumuisha taratibu za kitaasisi, uwajibikaji, uongozi, mbinu za majadiliano, maarifa, na ushirikishaji wa umma.

**Hivyo, matokeo** ya kazi yetu yanahu maeneo muhimu ya taasisi, ujumuishi, na taarifa kama ifuatavyo:

### Taasisi

- Kuhakikisha kuwa jamii zina umiliki salama wa ardhi na upatikanaji wa maliasili
- Kuimarisha utambuzi wa haki za ardhi kwa wanawake na vijana
- Kuimarisha mbinu za kijamii za usuluhishi wa migogoro kwa uwazi zaidi na ubayana wa kisheria
- Kuchochea haki katika mbinu za kugawana faida na kuchangia gharama katika ngazi ya jamii
- Kuunga mkono na kuruhusu jamii kuwa na muda wa kupata uzoefu na kuanza kutumia njia mpya za kusimamia maliasili zao

### Ujumuishi

- Kuhakikisha kuna ushiriki jumuishi wa makundi maalum katika ufanyaji maamuzi kuhusu matumizi ya ardhi
- Kuimarisha mkabala wa kiushirikiano katika matumizi endelevu ya ardhi
- Kusaidia ujenzi wa muda mrefu wa uwezo wa jamii kwa kutumia jumuiya za kiraia na ngazi za kati za kitaifa

### Taarifa

- Kupanua upatikanaji na uwepo wa taarifa za matumizi ya ardhi katika ngazi za chini (ICT)
- Kuboresha utunzaji kumbukumbu za kitaasisi kuhusu usimamizi wa maliasili katika ngazi za wilaya na jamii, hususani kuitia benki za taarifa zinazohusu ardhi katika vitengo vyote vyta kuitawala.

# MUHTASARI WA KISERA

## Wajibu wa Kimataifa, uwajibikaji ndani ya nchi



**Irmeli Mustalahti**, University of Eastern Finland, Finland - Chuo Kikuu cha Ufini Mashariki, Ufini

**Bernadeta Killian**, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

**Arun Agrawal**, University of Michigan, USA - Chuo Kikuu cha Michigani, Marekani

**Antti Erkkilä**, University of Eastern Finland, Finland - Chuo Kikuu cha Ufini Mashariki, Ufini

**Bishnu Devkota**, Tribhuvan University, Nepal - Chuo Kikuu cha Tribhuvan, Nepali

**Maija Hyle**, University of Eastern Finland, Finland - Chuo Kikuu cha Ufini Mashariki, Ufini

**Violeta Gutiérrez Zamora**, University of Eastern Finland, Finland - Chuo Kikuu cha Ufini Mashariki, Ufini

**Aristarik Hubert Maro**, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Tanzania

**Dismas Lyegendili Mwaseba**, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Tanzania

**Gimbage Mbeyale**, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Tanzania

**Papa Faye**, Action Research and Development Centre, Senegal - Kituo cha Utafiti na Maendeleo, Senego

**Edda Tandi Lwoga**, Chuo cha Elimu ya Biashara, Tanzania

**Usimamizi wa Kiuwajibikaji wa Maliasili  
Kikundi cha Utafiti kimegharimiwa na Akademia ya Ufini**

[antti.erkkila\(at\)uef.fi](mailto:antti.erkkila(at)uef.fi)

[irmeli.mustalahti\(at\)uef.fi](mailto:irmeli.mustalahti(at)uef.fi)

[www.uef.fi/responsive-natural-resources-governance](http://www.uef.fi/responsive-natural-resources-governance)

